

## 13H-As-Sakt - Kipumziko

### السَّكْتُ As-Sakt - Kipumziko

Ni kipumziko (kunyamaza) katika kusoma neno la Qur-aan kadiri ya harakah mbili bila ya kushush pumzi kwa nia ya kuendelea katika kusoma. Sababu ya kupumzika: kwa ujumla ni kwa ajili ya kuepusha utatanishi wa maana; kama hutosimama huenda ikafahamika maana isiyokusudiwa.

Alama yake ni herufi ya س

Katika riwaayah ya Hafsw 'an 'Aaswim, sehemu nne ni وَاجِب (waajib) (imewajibika) na mbili ni خَانِزٌ jaaiz (inaruhusika). Zilizokuwa وَاجِب (waajib) ni:

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي أَنْزَلَ عَلَى عَبْدِهِ الْكِتَابَ وَلَمْ يَجْعَلْ لَهُ عِوْجَانًا قِيمًا لِّيُنْذِرَ بَاسًا شَدِيدًا<sup>1</sup>

قَالُوا يَنْوَيْلَنَا مَنْ بَعَثَنَا مِنْ مَرْقَدِنَا هَذَا مَا وَعَدَ الرَّحْمَنُ وَصَدَقَ الْمُرْسَلُونَ<sup>2</sup>

وَقِيلَ مَنْ رَاقٍ<sup>3</sup>

Bonyeza usikilize

كَلَّا كَلَّا رَانَ عَلَى قُلُوبِهِمْ مَا كَانُوا يَكْسِبُونَ<sup>4</sup>

Bonyeza usikilize

<sup>1</sup>Al-Kahf (18: 1-2)

<sup>2</sup>Yaasiyn (36 : 52)

<sup>3</sup>Al-Qiyaamah (75 : 27)

<sup>4</sup>Al-Mutwaffifiyn (83 : 14)

Zilizokuwa جائز (jaaiz) ni:

س  
مَا أَغْنَى عَنِي مَالِيَهُ هَلَكَ عَنِي سُلْطَانِيَهُ<sup>٥</sup>

إِنَّ اللَّهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ<sup>٦</sup> بَرَآءَةٌ مِنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ إِلَى الَّذِينَ عَاهَدْتُم مِنَ الْمُشْرِكِينَ<sup>٧</sup>

Katika hali ya kuunganisha Suwrah Al-Anfaal na Suwrah At-Tawbah msomaji atatakiwa apumzike hapo kipumziko kadiri ya harakah mbili bila ya kushusha pumzi. Pamoja na hivyo, hapa panajuzu au panafaa kusomwa kwa njia tatu tofauti; القطع (Al-Qatw'u), السكت (As-Sakt) na الوصل (Al-Wasl) kwa maana:

1. **القطع** (Al-Qatw'u): Ni kusoma kwa kusimama mwishoni mwa Aayah kwa kuleta 'aaridhw as-sukuwn katika 'Aliyym. Kisha kuanza Aayah inayofuatia:

*Innaa Allaaha bikulli shay-in 'Aliyyym. Baraatum-mina-Allaahi....*

2. **السكت** (As-Sakt): Kupumzika katika mwisho wa Aayah kwa kadiri ya haraka mbili bila ya kushusha pumzi kisha kuendeleza Aayah inayofuatia:

*Innaa Allaaha bikulli shay-in 'Aliym السكت Baraatum-mina-Allaahi....*

---

<sup>5</sup>Al-Haaqqah (69: 28-29)

<sup>6</sup> Al-Anfaal (8: 75)

<sup>7</sup> At-Tawbah (9: 1)

3. الْوَصْلُ (Al-Waswl): Kuunganisha Aayah ya kwanza na ya pili yake bila ya kusimama na kutekeleza hukmu ya Tajwiyd inayopasa mwishoni mwa Aayah ya mwanzo na kinachofuatia cha Aayah ya pili; yaani

*Innaa Allaaha bikulli shay-in 'Aliymum-baraatum-mina-Allaahi... ...*